

136 *Ufalme Umeanza Kutawala* *—Na Uje!* (Ufunuo 11:15; 12:10)

1. Yehova, tangu zamani,
Daima upo tu.
Mwana wako atawala;
Kwa agizo lako.
Ufalme umezaliwa;
Utatawala dunia.

(KORASI)

*Sasa kumekuwa
Wokovu nguvu ufalme.
Umeshazaliwa.
Basi: “Na uje, Na uje!”*

2. Shetani muda wafika;
Asiwepo tena.
Japo nyakati hatari,
Sisi si vipofu.
Ufalme umezaliwa;
Utatawala dunia.

(Korasi)

3. Malaika wana shangwe
Shetani katupwa.
Uwongo wake haupo
Mbingu zatulia.
Ufalme umezaliwa;
Utatawala dunia.

(Korasi)